

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA TATU

04 APRILI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA TATU – TAREHE 04 APRILI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

28. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kulipatia Jimbo la Busanda Halmashauri kwani michakato ya DCC na RCC iliwasilishwa TAMISEMI.

29. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itawalipa posho Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji na kuongeza posho ya Madiwani ili kuwasaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

30. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kumaliza tatizo la uhaba wa Walimu kwa Shule za Sekondari na za Msingi katika Wilaya ya Ikungi.

WIZARA YA NISHATI:

31. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itaweka Bomba la gesi kila nyumba Jijini Dar es Salaam ili Wananchi wapikie nishati nafuu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

32. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka Walimu katika Chuo cha VETA Kitangari ili kuleta ufanisi wa elimu inayotolewa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

33. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kununua Magari ya Zimamoto kwa ajili ya Kituo cha Zimamoto na Uokoaji Mchicha - Temeke.

WIZARA YA UJENZI:

34. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mkandarasi wa Barabara ya Lupilo, Malinyi, Kilosa kwa Mpepo hadi Londo ataanza kazi kwa mtindo wa EPC + F.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

35. MHESHIMIWA SEIF SAID KHAMIS GULAMALI (MANONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni adhabu gani inatolewa kwa Watumishi wa Wakala wa Huduma za Mimitu (TFS) wanaobainika kudhuru raia na mali zao.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

36. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua Viwanda vilivyokufa katika Mkoa wa Tanga.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

37. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kituo cha Madume Bora ya Ng'ombe Wilayani Bahi.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI MKUU:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
04 APRILI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**